

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



S.L.P 1951Moshi-Kilimanjaro
Simu : 027-2750885 Nukushi :027- 2750889
Barua pepe: rbckilimanjaro@pccb.go.tz
Wavuti www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

**MHASIBU NA AFISA UTUMISHI WA HALMASHAURI YA ROMBO
MAHAKAMANI KWA UBADHILIFU WA ZAIDI YA MILIONI TISINI**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro imewafungulia mashtaka katika Mahakama ya Wilaya ya Rombo aliyekuwa Mhasibu wa Halmashauri ya Wilaya hiyo Robert Ndomele Msuka na Aliyekuwa Afisa Utumishi Edson Nkondora kwa makosa ya kutumia nyaraka kumudanganya mwajiri na ubadhirifu wa fedha za umma.

Kesi hiyo ya Jinai Namba CC. 1/2018 inayohusisha ubadhirifu wa shilingi tisini na tano milioni thelathini na moja elfu mia nne thelathini na tano (Tzsh. 95,031,435/=) ipo mbele ya hakimu mfawidhi wa mahakama hiyo msheshimiwa Regina Futakamba na imefikishwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU Rehema Mteta.

Ndomele ambaye kwa sasa ni Mhasibu wa Halmashauri ya Misenyi na Nkondora ambaye kwa sasa ni Afisa Utumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha, wameunganishwa na Veneranda Marcel Mosha (mtunza fedha wa Halmashauri ya Rombo) na Godfrey Mwakalinga ambaye alikuwa dereva wa Halmashauri ya Rombo na sasa ameachishwa kazi.

Katika shtaka la kwanza Kondora, Ndomele na Veneranda wanashtakiwa kwa kutumia nyaraka za udanganyifu kuonyesha kuwa fedha (Tshs. 67,200,000/=) zilitumika kukodi magari kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2015, huku uchunguzi ukionyesha kwamba, nyaraka waliyowasilisha kuhalalisha matumizi ya fedha hizo ina Namba za magari ya Serikali, Malori, pikipiki na Namba ambazo hazijawahi kuwemo katika mfumo wa usajali wa vyombo vya moto wa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Katika shtaka la pili Kondora, Ndomele na Veneranda wanashtakiwa kwa kutumia nyaraka za udanganyifu kuonyesha kwamba (Tshs. 8,680,000/=) zilitumika kulipa Kampuni ya LUDO INVESTMENT MEAT LIMITED kwa ajili ya matangazo ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, huku wakifahamu haikuwa kweli.

Katika shtaka la tatu, Kondora, Ndomele na Veneranda, wanashtakiwa kwa kutumia nyaraka kudanganya kuwa (Tshs. 750,000/=) zilitumika kulipia ukumbi Shule ya Sekondari Shauritanga kwa ajili ya mafunzo ya wasimamizi wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, huku wakifahamu kuwa haikuwa kweli.

Katika shtaka la nne Kondora, Ndomele na Veneranda wanashtakiwa kwa kuwasilisha nyaraka za udanganyifu kuonyesha kuwa (Tshs. 18,401,435/=) walilipa Kampuni ya B. J. SHIRIMA Catering Services kwa ajili ya chakula na viburudisho katika Semina ya Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi Mkuu wa 2015, huku wakijua sio kweli.

Shtaka la tano linamhusu Godfrey Meck Mwakalinga ambaye hakuwepo mahakamani, anashtakiwa kwa kutumia nyaraka kudanganya kuwa (Tshs.575,565/=) zilitumika kununua mafuta ya disel lita 250 kwa ajili ya gari SM10300 kituo cha mafuta kiitwacho TILISHO PETROL STATION kwa ajili ya matumizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, huku akijua kuwa hakuwahi kununua mafuta hayo.

Katika shtaka la sita Nkondola, Ndomele na Veneranda wanashtakiwa kwa ubadhirifu wa fedha (Tshs. 95,031,435/=) zilizokuwa zimetengwa kwa shughuli za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, kinyume cha k/f cha 28 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007, Washtakiwa wote wamekana mashtaka yao na wameshindwa kutimiza masharti ya zamana na hivyo wamepelekwa mahabusu hadi tarehe 22/11/2018 kesi hiyo itakapotajwa tena.

Hati ya kuitwa mshtakiwa Godfrey Meck Mwakalinga imetolewa na mahakama na anatakiwa kufika mahakamani hapo tarehe 22/11/2018 bila kukosa.

Holle Makungu
Mkuu wa TAKUKURU (M) Kilimanjaro
8 Novemba 2018